

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

**BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA
NISHATI NA MAJI (EWURA CCC)**



**MAONI YA BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA CCC) JUU YA OMBI LA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
IGUNGA (IGUWASA) LA MAPITIO YA BEI ZA HUDUMA ZA MAJISAFI NA USAFI WA
MAZINGIRA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO KUANZIA 2026/27–2030/31**

1. Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA Consumer Consultative Council - EWURA CCC) linapenda kuwasilisha maoni yake kuhusu ombi la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Igunga (IGUWASA) la kutaka kuidhinishiwa bei mpya za huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka wa fedha 2026/27 hadi 2030/31.

Maoni haya yametokana na mapitio ya nyaraka zilizowasilishwa na IGUWASA pamoja na Kanuni husika za EWURA, zikiwemo:

- i. Ombi la Mapitio ya Bei 2026/27–2030/31 (Tariff Application);
- ii. Mpango Biashara ulioidhinishwa wa miaka mitano 2026/27–2030/31 (Approved Business Plan);
- iii. Mkataba wa Utendaji kati ya Wizara ya Maji na IGUWASA (Performance Contract);
- iv. Muhtasari wa Kikao Maalumu cha Bodi cha tarehe 21 Mei 2026 kilichojadili marekebisho ya bei za huduma za majisafi na usafi wa mazingira;
- v. Muhtasari wa Kikao cha Wadau wa Maji cha tarehe 26 Mei 2026 kuhusu mchakato wa marekebisho ya bei;
- vi. Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa miaka iliyoishia tarehe 30 Juni 2024 na tarehe 30 Juni 2025;

- vii. Barua ya Wizara ya Maji ya kutokuwa na pingamizi kuhusu ombi la IGUWASA la mapitio ya bei; na
 - viii. The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Water Tariff Application and Rate Setting) Rules, 2020, GN No. 490.
2. IGUWASA inapendekeza kuongeza bei ya maji kwa matumizi ya majumbani kutoka Shilingi 1,666 kwa mita ya ujazo hadi Shilingi 3,233 kwa mita ya ujazo mwaka 2026/27. Kwa kundi la taasisi, bei inapendekezwa kuongezeka kutoka Shilingi 1,850 hadi Shilingi 3,591 kwa mita ya ujazo; biashara kutoka Shilingi 2,900 hadi Shilingi 5,628; viwanda kutoka Shilingi 2,330 hadi Shilingi 4,522; na vioski kutoka Shilingi 1,500 hadi Shilingi 2,911 kwa mita ya ujazo. Kwa ujumla, bei zinazopendekezwa kwa makundi hayo zinaonesha ongezeko la takribani asilimia 94 katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji ikilinganishwa na bei za sasa (Ombi la Marekebisho ya Bei, Jedwali Na. 3, uk. 7).

Pamoja na manufaa yanayotarajiwa kutokana na marekebisho ya bei yaliyoainishwa katika nyaraka za IGUWASA, ikiwemo kuimarisha uendelevu wa kifedha wa Mamlaka, kuboresha na kupanua huduma, nyaraka hizo pia zinaeleza umuhimu wa kuwa na marekebisho ya bei ya taratibu na yanayotabirika ili kupunguza athari za ongezeko kubwa la ghafla kwa watumiaji (Ombi la Marekebisho ya Bei, Executive Summary, uk. vii; Jedwali Na. 2, uk. 7).

Hata hivyo, ongezeko linalopendekezwa la takribani asilimia 94 lilipingwa na wadau kutokana na athari zake katika uwezo wa wananchi kumudu huduma, ambapo ilipendekezwa ongezeko lisizidi asilimia 50 na litekelezwe kwa awamu. Hivyo, pamoja na kutambua umuhimu wa marekebisho ya bei kutokana na ongezeko la gharama za utoaji wa huduma, hoja kuu ya wadau ilikuwa kupunguza athari ya ongezeko kubwa la mara moja kwa watumiaji (Muhtasari wa Kikao cha Wadau cha tarehe 26 Mei 2026, uk. 3–6).

Baraza linatambua kuwa IGUWASA inahitaji mapato ya kutosha kugharamia uendeshaji, matengenezo na uwekezaji muhimu kwa ajili ya utoaji wa huduma endelevu. Hata hivyo, ongezeko la takribani asilimia 94 katika mwaka wa kwanza ni

kubwa na linaweza kuathiri uwezo wa watumiaji kumudu huduma. Aidha, kiwango hicho kinahitaji kutazamwa kwa kuzingatia dhamira ya kuwa na marekebisho ya bei ya taratibu na yanayotabirika. Hivyo, ni muhimu kujiridhisha iwapo Mahitaji ya Mapato yanayostahili yanahitaji ongezeko lote hilo katika mwaka wa kwanza, au kama sehemu yake inaweza kusambazwa katika kipindi cha bei bila kuathiri uendelevu wa huduma.

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuhakiki kwa kina Mahitaji ya Mapato ya IGUWASA ili kujiridhisha kuwa kiwango cha ongezeko la bei kinatokana na gharama zilizothibitishwa kuwa za lazima, zenye ufanisi na zinazohitajika katika utoaji wa huduma;
 - ii. Baada ya kubaini Mahitaji ya Mapato yanayostahili, kutathmini upya kiwango cha ongezeko la mwaka wa kwanza na uwezekano wa kulitekeleza kwa awamu, ili kupunguza athari ya ongezeko kubwa la mara moja kwa watumiaji bila kuhatarisha uendelevu wa huduma;
 - iii. Kuzingatia uwezo wa watumiaji kumudu huduma pamoja na maoni ya wadau kuhusu kiwango cha ongezeko; na
 - iv. Kuhakikisha kuwa bei itakayoidhinishwa inaweka uwiano unaofaa kati ya uwezo wa watumiaji kumudu huduma na uendelevu wa kifedha wa IGUWASA
3. IGUWASA imeainisha ongezeko la gharama za uzalishaji wa maji kuwa miongoni mwa sababu kuu za kuomba marekebisho ya bei. Gharama za ununuzi wa maji kwa jumla zinatarajiwa kuongezeka kutoka Shilingi bilioni 1.39 mwaka 2025/26 hadi Shilingi bilioni 3.09 mwaka 2030/31, sawa na ongezeko la takribani asilimia 122. Gharama za kemikali nazo zinatarajiwa kuongezeka kutoka Shilingi milioni 237.0 hadi Shilingi milioni 703.5, sawa na ongezeko la takribani asilimia 197 katika kipindi hicho. Aidha, IGUWASA imeainisha ongezeko la gharama za umeme pamoja na gharama zinazohusiana na hatua za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. (Ombi la Marekebisho ya Bei, Sehemu ya 2.1, uk. 3; Jedwali Na. 8, uk. 11).

Gharama za watumishi zinatarajiwa kuongezeka kutoka Shilingi bilioni 1.21 mwaka 2025/26 hadi Shilingi bilioni 2.50 mwaka 2030/31, sawa na ongezeko la takribani asilimia 106. Mbali na gharama hizo, IGUWASA imekadiria gharama nyingine za

utawala na uendeshaji, zikiwemo mafunzo ya watumishi, bima, mawasiliano, mafuta na usafiri (Ombi la Marekebisho ya Bei, Sehemu ya 2.4, uk. 4–5; Jedwali Na. 8, uk. 11–12).

Baraza linatambua kuwa baadhi ya gharama za uzalishaji, hususan ununuzi wa maji kwa jumla, kemikali na umeme, ni muhimu ambazo Mamlaka haiwezi kuziepuka bila kuathiri uzalishaji na ubora wa huduma. Hivyo, suala la msingi kwa gharama hizo ni kujiridhisha kuwa makadirio yake yanaendana na kiasi cha maji kinachotarajiwa kuzalishwa au kununuliwa, bei husika za pembejeo na mahitaji halisi ya uendeshaji.

Hata hivyo, Baraza linaona haja ya kuwa na uhakiki mkali zaidi wa gharama ambazo Mamlaka ina uwezo mkubwa wa kuzidhibiti, hususan gharama za watumishi na matumizi ya kiutawala. Ongezeko la gharama za watumishi kutoka Shilingi bilioni 1.21 hadi Shilingi bilioni 2.50, sawa na asilimia 106, linahitaji maelezo ya kutosha kuhusu sababu zinazofanya gharama hizo zaidi ya kuongezeka mara mbili katika kipindi cha miaka mitano. Aidha, gharama za mafunzo, mafuta, usafiri, mawasiliano na matumizi mengine ya kiutawala zinapaswa kutathminiwa kwa kuzingatia umuhimu wake katika utoaji wa huduma na fursa zilizopo za kudhibiti matumizi.

Baraza linaona kuwa si kila ongezeko la matumizi ya ndani ya Mamlaka linapaswa kuhamishiwa moja kwa moja kwa watumiaji kupitia bei. Kabla ya gharama hizo kujumuishwa kikamilifu katika Mahitaji ya Mapato, IGUWASA inapaswa kuonesha kuwa ongezeko hilo ni la lazima, lina uhusiano na mahitaji ya utoaji wa huduma, na haliwezi kupunguzwa kupitia maboresho ya ufanisi. Hii ni muhimu zaidi katika mazingira ambayo watumiaji wanakabiliwa na pendekezo la ongezeko la bei la takribani asilimia 94 katika mwaka wa kwanza.

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuhakiki makadirio ya gharama za ununuzi wa maji, kemikali na umeme kwa kuzingatia kiasi kinachotarajiwa kutumika na bei husika, ili kujiridhisha kuwa ongezeko lililokadiriwa linaendana na mahitaji halisi ya utoaji wa huduma;

- ii. Kuitaka IGUWASA kutoa mchanganuo wa sababu za ongezeko la gharama za watumishi kwa asilimia 106, ukionesha mchango wa ajira mpya, nyongeza za mishahara, kupandishwa vyeo, posho na michango ya mwajiri katika ongezeko hilo;
 - iii. Kuhakiki kwa kina gharama za utawala na uendeshaji, hususan mafunzo, mafuta, usafiri, mawasiliano na matumizi mengine yanayoweza kudhibitiwa, na kuruhusu kiwango kinachothibitishwa kuwa muhimu katika utoaji wa huduma;
 - iv. Kulinganisha gharama zinazopendekezwa na matumizi halisi ya miaka iliyopita ili kubaini maeneo ambayo yana nafasi ya kuongeza ufanisi na kupunguza shinikizo la gharama kwa watumiaji; na
 - v. Kuhakikisha kuwa Mahitaji ya Mapato yanajumuisha gharama halali na muhimu za uzalishaji pamoja na kiwango cha gharama za ndani kinachofaa na chenye ufanisi, badala ya kuhamisha moja kwa moja ongezeko lote la matumizi kwa watumiaji.
4. IGUWASA ilitekeleza kikamilifu baadhi ya masharti ya Agizo la Bei lililopita, ikiwemo ukarabati wa njia ya kupitisha maji ya ziada (spillway) ya Bwawa la Bulenya, ujenzi wa mnara mpya wa uwekaji klorini pamoja na ubadilishaji wa tanki la zamani la uwekaji klorini. Utekelezaji huo ni hatua chanya kwa kuwa shughuli hizo zililenga kuboresha na kuendeleza huduma ya maji (Ombi la Marekebisho ya Bei, Jedwali Na. 1, uk. 6).

Hata hivyo, baadhi ya masharti hayakutekelezwa kikamilifu. IGUWASA ilibadilisha mita chakavu na zisizo sahihi 959, sawa na asilimia 70 ya lengo, na kununua mita mpya 2,773, sawa na asilimia 93.6 ya lengo. Aidha, Mamlaka ilipata ekari 12.4 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya majitaka na kinyesi dhidi ya lengo la ekari 50, na kupanua mtandao kwa kilomita 3.3 dhidi ya kilomita 4 zilizopangwa. Mabomba yenye ukubwa wa 300mm, 225mm na 150mm yenye jumla ya kilomita 2 hayakubadilishwa, ambapo IGUWASA imeeleza kuwa sababu ilikuwa kuchelewa kupata bei ya sasa ya maji (Ombi la Marekebisho ya Bei, Jedwali Na. 1, uk. 6).

Wakati huo, ombi jipya linajumuisha shughuli zinazohusiana na maeneo ambayo baadhi ya malengo ya awali hayakufikiwa, ikiwemo upanuzi wa mtandao, ufungaji wa mita kwa wateja wapya, ubadilishaji wa mita zisizo sahihi na ukarabati wa mabomba chakavu. IGUWASA inapanga kuweka kilomita 40 za mabomba ya HDPE, kufunga mita 4,000 kwa wateja wapya na kubadilisha mita zisizo sahihi 11,950, pamoja na kufanya ukarabati wa miundombinu ya usambazaji (Ombi la Marekebisho ya Bei, Sehemu ya 2.3.1–2.3.2, uk. 4).

Baraza linatambua kuwa kutotekelezwa kwa shughuli zote katika kipindi kilichopita hakumaanishi kuwa shughuli hizo hazihitajiki tena. Baadhi zinaweza kuwa muhimu zaidi sasa kutokana na hali ya miundombinu na mahitaji ya huduma. Hata hivyo, kwa kuwa baadhi ya shughuli zinazofanana zimejumuishwa katika ombi jipya, ni muhimu kufanya upatanisho (reconciliation) ya fedha na kazi zilizotekelezwa ili kuhakikisha kuwa watumiaji hawalipii mara mbili gharama ambayo tayari ilizingatiwa katika bei ya kipindi kilichopita.

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuitaka IGUWASA kueleza sababu za kutokamilika kwa shughuli muhimu zilizoinishwa katika Agizo la Bei lililopita na kuonesha kiasi cha fedha kilichotengwa, kilichotumika na kazi iliyobaki;
- ii. Kulinganisha shughuli ambazo hazikukamilika na shughuli zinazopendekezwa katika Mpango mpya wa Uwekezaji ili kubaini kama gharama hizo zimeingizwa tena katika ombi la sasa;
- iii. Pale ambapo shughuli ya awali bado ni muhimu na inapaswa kuendelea, kuruhusu gharama halisi iliyobaki kutekeleza shughuli hiyo, baada ya kuzingatia kiasi chochote ambacho tayari kilifadhiliwa katika kipindi kilichopita; na
- iv. Kuhakikisha kuwa shughuli ambazo tayari zimekamilika au kugharamiwa hazijumuishwi tena katika Mahitaji ya Mapato ya kipindi kipa.

5. Makadirio ya Mahitaji ya Mapato ya IGUWASA yanaonesha ongezeko kubwa katika mwaka wa kwanza wa kipindi cha bei. Gharama za uendeshaji na matengenezo zinakadiriwa kuongezeka kutoka takribani Shilingi bilioni 3.878 mwaka 2025/26 hadi Shilingi bilioni 6.683 mwaka 2026/27, sawa na ongezeko la takribani asilimia 72.3. Gharama za uchakavu nazo zinaongezeka kutoka takribani Shilingi milioni 776.9 hadi Shilingi milioni 893.2, sawa na ongezeko la takribani asilimia 15. Aidha, katika mwaka 2026/27 Mahitaji ya Mapato yanajumuisha marejesho ya uwekezaji (ROI) ya takribani Shilingi bilioni 1.956, na kufanya jumla ya Mahitaji ya Mapato kufikia takribani Shilingi bilioni 9.533. Baada ya kutoa mapato mengine, takribani Shilingi bilioni 9.491 zinatarajiwa kurejeshwa kupitia mauzo ya maji. (Ombi la Marekebisho ya Bei, Jedwali Na. 16, uk. 23).

Ukubwa wa ongezeko hilo la gharama unaonekana pia katika bei inayopendekezwa kwa watumiaji. Bei ya wastani yenye uzito (Weighted Average Tariff) inapendekezwa kuongezeka kutoka Shilingi 3,167 hadi Shilingi 6,145 kwa mita ya ujazo mwaka 2026/27, sawa na ongezeko la takribani asilimia 94.0. Vilevile, kama ilivyoainishwa katika Hoja ya 2, bei za makundi makuu ya watumiaji zinaongezeka kwa kiwango kinachokaribia asilimia 94 katika mwaka huo wa kwanza. (Ombi la Marekebisho ya Bei, Jedwali Na. 3, uk. 7–8).

Baraza linatambua kuwa gharama za uendeshaji na matengenezo, uchakavu wa mali na marejesho ya uwekezaji ni vipengele vinavyoweza kuzingatiwa katika Mahitaji ya Mapato. Hata hivyo, ongezeko la gharama za uendeshaji na matengenezo (O&M) la asilimia 72.3, kuingizwa kwa ROI ya takribani Shilingi bilioni 2 na matokeo yake katika ongezeko la bei ya wastani yenye uzito (Weighted Average Tariff) la takribani asilimia 94 katika mwaka mmoja vinaonesha umuhimu wa kufanya uhakiki wa kina wa Mahitaji ya Mapato kabla ya gharama hizo kuhamishiwa kwa watumiaji. Kanuni za EWURA zinaelekeza kwamba gharama za O&M zinazokubalika zinapaswa kuwa gharama zilizotumika kwa haki, kwa uangalifu na kwa ufanisi katika utoaji wa huduma inayodhibitiwa. (EWURA Water Tariff Application and Rate Setting Rules, 2020, Kanuni ya 31, uk. 26).

Katika sehemu ya marejesho ya uwekezaji, IGUWASA imeonesha Msingi wa Mali (Rate Base) wa Shilingi bilioni 17.937 mwaka 2026/27, inayoongezeka hadi Shilingi bilioni 18.486 mwaka 2030/31. Hata hivyo, Jedwali Na. 12 linaonesha Wastani wa Gharama za Mtaji (WACC) kama “0.0” katika miaka yote, wakati jedwali hilo linaonesha Marejesho ya Uwekezaji (ROI) ya Shilingi bilioni 1.783 mwaka 2026/27 hadi Shilingi bilioni 1.838 mwaka 2030/31. Kwa kuwa ROI imeelezwa kukokotolewa kwa kutumia $WACC \times Rate\ Base$, kutokuwepo kwa kiwango cha WACC kinachoonekana katika jedwali kunafanya msingi wa ukokotoaji wa ROI kutokuwa wazi na hivyo kuhitaji ufafanuzi kabla ya marejesho hayo kuruhusiwa katika bei. (Ombi la Marekebisho ya Bei, Sehemu ya 9 na Jedwali Na. 12, uk. 17–18).

Kanuni zinaelekeza kuwa Rate Base inapaswa kujumuisha mali zinazotumika katika shughuli zinazodhibitiwa, huku ruzuku na michango ya wahusika wengine ikiondolewa. Aidha, EWURA inaweza kuhitaji ushahidi kwamba mali zilizojumuishwa katika Rate Base zilibuniwa, kununuliwa au kujengwa kwa uangalifu unaostahili. (EWURA Water Tariff Application and Rate Setting Rules, 2020, Kanuni ya 43, uk. 29).

Baraza linaona kuwa suala hili lina uzito mkubwa kwa watumiaji kwa sababu kila ongezeko lisilothibitishwa katika Mahitaji ya Mapato (Revenue Requirement) lina athari katika bei inayopaswa kulipwa. Hivyo, iwapo gharama za uendeshaji na matengenezo (O&M), Rate Base au ROI itaruhusiwa kwa kiwango kikubwa kuliko kinachostahili, watumiaji wanaweza kubebeshwa ongezeko la bei lisilotokana kikamilifu na gharama halali za utoaji wa huduma. Zaidi ya hapo, Kanuni ya 46 inaruhusu EWURA kufanya usawazishaji wa Mahitaji ya Mapato katika kipindi cha bei cha miaka mitano kwa kupanga upya uwekezaji ili kuepusha mshtuko au mabadiliko makubwa ya bei kwa watumiaji (EWURA Water Tariff Application and Rate Setting Rules, 2020, Kanuni ya 46, uk. 30).

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kufanya uhakiki wa kina wa Mahitaji ya Mapato ya IGUWASA, hususan ongezeko la gharama za uendeshaji na matengenezo (O&M) la takribani asilimia

72.3 katika mwaka 2026/27, na kuruhusu gharama zilizothibitishwa kuwa za lazima, za kiwango kinachofaa na zenye ufanisi pekee;

- ii. Kuitaka IGUWASA kuwasilisha kiwango halisi cha WACC kilichotumika kukokotoa ROI, pamoja na mchanganuo unaowezesha kuthibitisha ROI iliyojumuishwa katika Mahitaji ya Mapato, kwa kuwa Jedwali Na. 12 halioneshi kiwango hicho kwa uwazi;
 - iii. Kuhakiki Rate Base ya Shilingi bilioni 17.937 na kujiridhisha kuwa inajumuisha mali zinazostahili kutumika kukokotoa marejesho ya uwekezaji, huku ruzuku na michango ya wahusika wengine ikishughulikiwa kwa mujibu wa Kanuni;
 - iv. Baada ya uhakiki wa gharama za uendeshaji na matengenezo (O&M), uchakavu, Rate Base na ROI, kukokotoa upya Mahitaji ya Mapato na kiwango cha bei kinachostahili, badala ya kuruhusu moja kwa moja ongezeko la bei ya wastani yenye uzito (Weighted Average Tariff) la takribani asilimia 94; na
 - v. Iwapo Mahitaji ya Mapato yaliyothibitishwa bado yatasababisha ongezeko kubwa la bei katika mwaka wa kwanza, kutumia uwezekano unaotolewa na Kanuni ya 46 wa kusawazisha Mahitaji ya Mapato katika kipindi cha bei, ili kupunguza mshtuko wa bei kwa watumiaji bila kuhatarisha uendeleu wa kifedha wa IGUWASA.
6. Taarifa za IGUWASA zinaonesha kuwa Serikali imekuwa ikitoa ruzuku kwa ajili ya miradi ya maji na usafi wa mazingira. Katika kipindi cha nyuma, IGUWASA ilipokea takribani Shilingi milioni 611.15 mwaka 2022/23, Shilingi milioni 612.47 mwaka 2023/24 na Shilingi bilioni 1.433 mwaka 2024/25. Fedha hizo zilitumika katika shughuli mbalimbali, zikiwemo upanuzi wa mtandao wa maji katika maeneo mbalimbali pamoja na ujenzi wa miundombinu ya majitaka na kinyesi katika Mji wa Igunga. Kwa kipindi kijacho, IGUWASA inatarajia kupokea ruzuku ya Shilingi milioni 631.5 mwaka 2026/27 na Shilingi milioni 631.5 mwaka 2027/28, mahsusi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu

ya kutibu majitaka na tope kinyesi katika Mji wa Igunga. (Ombi la Marekebisho ya Bei, Jedwali Na. 15, uk. 22).

Mpango Biashara unathibitisha kuwa mradi wa Kituo cha Kutibu Tope Kinyesi umepangiwa Shilingi milioni 631.5 mwaka 2026/27 na kiasi kama hicho mwaka 2027/28, na chanzo cha fedha kimeainishwa kuwa ruzuku. Aidha, Mpango Biashara unaonesha kuwa jumla ya uwekezaji wa miaka mitano ni takribani Shilingi bilioni 12.788 na unafadhiliwa kupitia mchanganyiko wa mapato ya ndani na ruzuku. (Business Plan, Jedwali Na. 14, uk. 30).

Mpango Biashara unaeleza zaidi kuwa vyanzo vya fedha vya IGUWASA vinajumuisha mapato ya ndani na ruzuku, ambapo ruzuku hutolewa hasa na Serikali kwa ajili ya miradi ya uwekezaji. Vyanzo vya nje vilivyoainishwa ni Serikali ya Tanzania, National Water Fund na Wizara ya Maji. (Business Plan, Sehemu ya 12.3–12.3.1, uk. 34).

Baraza linatambua na kuunga mkono matumizi ya ruzuku katika kugharamia miradi ya maji na usafi wa mazingira, kwa kuwa fedha hizo zinaweza kupunguza kiwango cha uwekezaji kinachopaswa kurejeshwa moja kwa moja kupitia bei zinazolipwa na watumiaji. Hata hivyo, manufaa hayo kwa watumiaji yanaweza kupungua iwapo mali iliyofadhiliwa kupitia ruzuku itajumuishwa katika msingi wa kukokotoa marejesho ya uwekezaji na hivyo kuruhusu Mamlaka kupata marejesho kupitia bei juu ya uwekezaji ambao umefadhiliwa na Serikali au wahusika wengine.

Jambo hili lina umuhimu zaidi kwa kuwa Kanuni za EWURA zinaelekeza moja kwa moja kuwa Rate Base inakokotolewa kwa fomula ya “ $RB = NCA - Grants + AWC$ ”, ambapo Grants (ruzuku) zinajumuisha ruzuku au michango ya wahusika wengine. Hivyo, ruzuku zinapaswa kuondolewa katika thamani ya mali inayotumika kukokotoa marejesho ya uwekezaji. (EWURA Water Tariff Application and Rate Setting Rules, 2020, Second Schedule, Item 4, uk. 51).

Pamoja na uwepo wa ruzuku hizo, nyaraka za IGUWASA hazijaonesha kwa uwazi upatanisho inayoweza kuthibitisha namna mali zilizofadhiliwa kupitia ruzuku

zilivyoshughulikiwa katika ukokotoaji wa Rate Base na ROI. Ombi la Marekebisho ya Bei limeainisha ruzuku katika Jedwali Na. 15 na, kwa upande mwingine, imekokotoa Rate Base na ROI katika sehemu tofauti; hivyo ni muhimu kujiridhisha kuwa thamani ya mali iliyofadhiliwa kupitia ruzuku imeondolewa ipasavyo katika Rate Base kabla ya kukokotoa marejesho yanayorejeshwa kupitia bei. (Ombi la Marekebisho ya Bei, Jedwali Na. 12, uk. 17–18; Jedwali Na. 15, uk. 22).

Baraza linaona suala hili ni muhimu katika kulinda maslahi ya watumiaji kwa sababu mtumiaji hapaswi kulipa marejesho ya uwekezaji juu ya sehemu ya mali ambayo tayari imefadhiliwa kupitia ruzuku ya Serikali au mchango wa mhusika mwingine. Ruzuku inapaswa kutoa manufaa halisi kwa watumiaji kwa kupunguza sehemu ya gharama za uwekezaji inayopaswa kurejeshwa kupitia bei, badala ya kuongeza marejesho inayotozwa kupitia tariff.

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha kuwa kila mradi mkubwa wa uwekezaji umeainishwa pamoja na chanzo chake cha fedha, kwa kutenganisha uwekezaji unaofadhiliwa kupitia mapato ya ndani ya IGUWASA na ule unaofadhiliwa kupitia ruzuku au michango ya wahusika wengine;
- ii. Kuhakiki Rate Base iliyotumika katika ukokotoaji wa ROI na kuhakikisha kuwa thamani ya mali iliyofadhiliwa kupitia ruzuku au michango ya wahusika wengine imeondolewa, kwa mujibu wa fomula ya Rate Base iliyoainishwa katika Second Schedule ya Kanuni;
- iii. Kuhakiki namna ruzuku ya Shilingi milioni 631.5 mwaka 2026/27 na Shilingi milioni 631.5 mwaka 2027/28 kwa ajili ya Kituo cha Kutibu Tope Kinyesi ilivyoshughulikiwa katika matumizi ya mtaji (CAPEX), Rate Base, Mahitaji ya Mapato (Revenue Requirement) na modeli ya bei;
- iv. Kuitaka IGUWASA kuwasilisha upatanisho wa Ruzuku-Matumizi ya Mtaji-Mali-Rate Base-ROI, ili kuthibitisha kuwa hakuna marejesho ya uwekezaji yanayokokotolewa juu ya mali iliyofadhiliwa kupitia ruzuku; na
- v. Kuhakikisha kuwa manufaa ya ruzuku yanaonekana katika kupunguza shinikizo la gharama kwa watumiaji na kuongeza upatikanaji na ubora wa

huduma, badala ya watumiaji kubebeshwa marejesho juu ya uwekezaji ambao tayari umefadhiliwa na Serikali au wahusika wengine.

7. Mpango wa Uwekezaji wa IGUWASA unakadiriwa kuwa na thamani ya jumla ya takribani Shilingi bilioni 12.788 katika kipindi cha miaka mitano. Miradi inayopangwa ni pamoja na upanuzi wa mtandao kwa kilomita 40 za mabomba ya HDPE, ujenzi na ukamilishaji wa kituo cha kutibu tope kinyesi, uwekezaji katika mita za maji za malipo kabla ya matumizi, hatua za kupunguza NRW kupitia ubadilishaji wa mita na uandaaji wa ramani za GIS, pamoja na ukarabati wa matenki, majengo, magari na miundombinu mingine chakavu. (Business Plan, Sehemu ya 11 na Jedwali Na. 14, uk. 30–32).

Baraza linatambua kuwa sehemu ya uwekezaji huo inaweza kutoa manufaa ya moja kwa moja kwa watumiaji. Kwa mfano, upanuzi wa mtandao unaweza kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma, ubadilishaji wa mita na ukarabati wa mabomba inaweza kusaidia kupunguza NRW, na ukarabati wa miundombinu unaweza kuongeza uhakika wa huduma. Hata hivyo, kwa kuwa sehemu ya gharama za uwekezaji inaweza kuathiri Mahitaji ya Mapato na hatimaye bei zinazolipwa na watumiaji, umuhimu wa mradi pekee hautoshi kuhalalisha gharama yake. Ni muhimu pia kujiridhisha kuwa mradi ni wa kipaumbele, gharama zake ni za kiwango kinachofaa, chanzo chake cha fedha kimeainishwa kwa usahihi na unaweza kutekelezwa ndani ya muda uliopangwa.

Jambo hili lina umuhimu zaidi kwa kuzingatia historia ya utekelezaji wa masharti ya Agizo la Bei lililopita, ambapo baadhi ya shughuli hazikukamilika kwa kiwango kilichopangwa, zikiwemo ubadilishaji wa baadhi ya mabomba, ubadilishaji wa mita, upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya miundombinu ya usafi wa mazingira na upanuzi wa mtandao. (Ombi la Marekebisho ya Bei, Jedwali Na. 1, uk. 6). Historia hiyo inaleta umuhimu wa kujiridhisha kuhusu uwezo wa IGUWASA kutekeleza Mpango mpya wa Uwekezaji kwa kiwango na muda uliopangwa, hususan pale ambapo gharama zake zinatarajiwa kuzingatiwa katika bei.

Baraza linaona watumiaji hawapaswi kubebeshwa kupitia bei gharama za miradi ambayo utekelezaji wake hauendani na ratiba au ambayo fedha zake hazitatumika

katika kipindi kilichokusudiwa. Kwa hiyo, shughuli ambazo hazikukamilika katika kipindi cha bei kilichopita zinahitaji kufanyiwa upatanisho ili kubaini kiasi kilichokusanywa, kiasi kilichotumika, shughuli zilizotekelezwa na salio lolote kabla ya mahitaji mapya ya fedha kwa shughuli hizo kuruhusiwa kupitia bei.

Aidha, Mpango Biashara umeweka malengo ya kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia 94.5 hadi asilimia 99, kupunguza NRW kutoka asilimia 22 hadi asilimia 17, kukamilisha mradi wa usafi wa mazingira na kuboresha ushughulikiaji wa malalamiko hadi asilimia 100. Malengo hayo yanatoa msingi wa kupima iwapo uwekezaji unaogharamiwa katika kipindi cha bei unaleta matokeo yaliyokusudiwa kwa watumiaji. (Business Plan, Jedwali Na. 12, uk. 27).

Hivyo, Baraza linaona kuwa tathmini ya Mpango wa Uwekezaji haipaswi kujikita katika ukubwa wa matumizi ya mtaji (CAPEX) pekee, bali pia katika vipaumbele vya miradi, uhalisia wa gharama, chanzo cha fedha, uwezo wa utekelezaji na matokeo yanayopimika kwa watumiaji. Miradi inayohitajika kwa mwendelezo wa huduma na uhakika wa huduma ya huduma, kupunguza NRW, kuboresha ubora wa huduma na kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma inapaswa kupewa kipaumbele. Miradi ambayo inaweza kuahirishwa au kutekelezwa kwa awamu bila kuathiri huduma inaweza kupangwa kwa namna inayopunguza shinikizo la gharama kwa watumiaji, hususan katika miaka ya mwanzo ya utekelezaji wa bei.

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kufanya tathmini ya kina ya Mpango wa Uwekezaji ili kujiridhisha kuwa miradi inayotarajiwa kurejeshewa gharama kupitia bei ni ya lazima, ya kipaumbele, ina gharama zinazostahili na inaweza kutekelezwa katika muda uliopangwa;
- ii. Kuitaka IGUWASA kuwasilisha ratiba ya kila mradi mkubwa inayoonesha gharama, chanzo cha fedha, mwaka wa utekelezaji, matokeo halisi ya utekelezaji na matokeo yanayotarajiwa kwa watumiaji, ili kuwezesha ufuatiliaji wa utekelezaji;
- iii. Kufanya upatanisho wa shughuli ambazo hazikukamilika chini ya Agizo la Bei lililopita, ikiwemo kiasi cha fedha kilichokusanywa au kutengwa, matumizi halisi

na kiwango cha utekelezaji, kabla ya gharama za shughuli hizo kuruhusiwa tena katika Mahitaji ya Mapato;

- iv. Kuhakikisha kuwa miradi inayofadhiliwa kupitia ruzuku au vyanzo vingine vya nje haitozwi tena kwa watumiaji kupitia bei, na inashughulikiwa ipasavyo katika matumizi ya mtaji (CAPEX), Rate Base na ROI;
 - v. Kuweka kipaumbele katika miradi yenye manufaa ya moja kwa moja na yanayopimika kwa watumiaji, hususan inayoongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma, kupunguza NRW na kuboresha uhakika wa huduma, mwendelezo wa huduma na ubora wa huduma;
 - vi. Pale ambapo kufanya hivyo hakuathiri utoaji wa huduma, kuzingatia kupanga utekelezaji wa baadhi ya miradi kwa awamu ili kupunguza shinikizo la gharama katika miaka ya mwanzo ya kipindi cha bei; na
 - vii. Kuweka utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa matumizi ya mtaji (CAPEX) dhidi ya malengo ya huduma, ili kuhakikisha kuwa fedha zinazorejeshwa kupitia bei zinatafsirika katika miradi iliyotekelezwa na maboresho halisi ya huduma kwa watumiaji
8. Mpango Biashara wa IGUWASA umeweka lengo la kupunguza kiwango cha maji yasiyoingiza mapato (Non-Revenue Water – NRW) kutoka asilimia 22 mwaka 2025/26 hadi asilimia 17 mwaka 2030/31. Taarifa za mwaka 2025/26 zinaonesha kuwa kiasi cha maji kilichoingia katika mfumo wa usambazaji kilikuwa mita za ujazo 1,867,715, wakati kiasi cha maji kilichotumiwa na wateja kilikuwa mita za ujazo 1,456,818, na hivyo kuacha tofauti ya mita za ujazo 410,897, sawa na asilimia 22 ya maji yaliyoingia katika mfumo. (Business Plan, Sehemu ya 2.2.15, uk. 11).

Ili kufikia lengo hilo, IGUWASA imeainisha hatua mbalimbali za kupunguza NRW, zikiwemo kubadilisha mita 11,950 zisizo sahihi, kuanzisha District Metered Areas (DMAs), kuandaa ramani za GIS za miundombinu na wateja pamoja na kukarabati mabomba chakavu ya usambazaji. Mpango wa Uwekezaji pia umejumuisha ubadilishaji wa mita na ukarabati wa miundombinu chakavu inayolenga kuongeza ufanisi wa mfumo na kupunguza NRW. (Ombi la Marekebisho ya Bei, Sehemu ya 2.3.2, uk. 4; Business Plan, Jedwali Na. 14, uk. 30–32).

Umuhimu wa kupunguza NRW unaonekana pia katika Mkataba wa Utendaji, ambao unaweka kiwango cha juu kinachokubalika cha NRW kuwa asilimia 20, huku kiwango cha msingi cha mwaka 2024/25 kikiwa asilimia 23 na lengo la mwaka 2025/26 likiwa asilimia 20. (Performance Contract, Appendix A, KPI 2.4, uk. 13).

Aidha, malengo ya kupunguza NRW yamejumuishwa moja kwa moja katika makadirio yaliyotumika kukokotoa Mahitaji ya Mapato na bei. Ombi la Marekebisho ya Bei limetumia dhana ya NRW kupungua kwa asilimia moja kila mwaka, kutoka asilimia 22 mwaka 2025/26 hadi asilimia 21 mwaka 2026/27, asilimia 20 mwaka 2027/28, asilimia 19 mwaka 2028/29, asilimia 18 mwaka 2029/30 na asilimia 17 mwaka 2030/31. Katika kipindi hicho, kiasi cha maji kinachotarajiwa kutozwa bili kinaongezeka kutoka mita za ujazo 1,456,818 hadi mita za ujazo 2,185,847. (Ombi la Marekebisho ya Bei, Jedwali Na. 16, uk. 23).

Baraza linatambua kuwa kupunguza NRW kuna manufaa ya moja kwa moja kwa watumiaji na kwa uendelevu wa IGUWASA, kwa kuwa kunapunguza upotevu wa rasilimali na kuongeza ufanisi wa mfumo wa usambazaji. Jambo la msingi zaidi ni kwamba makadirio ya mapato na bei ya IGUWASA yenyewe yamejengwa kwa kutegemea kufikiwa kwa malengo hayo ya NRW. Hivyo, malengo hayo hayapaswi kubaki kuwa makadirio ya kwenye nyaraka pekee, bali yanapaswa kuambatana na utekelezaji na matokeo yanayoweza kupimwa katika kipindi cha bei.

Kwa kuwa watumiaji wanatarajiwa kugharamia kupitia bei baadhi ya uwekezaji na hatua zinazolenga kupunguza NRW, Baraza linaona kuwa IGUWASA inapaswa pia kuwajibika kwa matokeo ya uwekezaji huo. Kutofikiwa kwa malengo ya NRW, hususan baada ya gharama za hatua zinazolenga kuipunguza kuruhusiwa kupitia bei, kunaweza kuwafanya watumiaji kubeba gharama bila kupata kikamilifu manufaa ya ufanisi yaliyotarajiwa. Aidha, kutofikiwa kwa malengo hayo kunaweza kuathiri dhana za kiasi cha maji kinachotarajiwa kutozwa bili na hivyo kuleta shinikizo zaidi katika Mahitaji ya Mapato na bei katika siku zijazo.

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuweka malengo ya kila mwaka ya kupunguza NRW kutoka asilimia 22 mwaka 2025/26 hadi asilimia 17 mwaka 2030/31 kama sehemu ya viashiria muhimu vya kufuatilia utekelezaji wa bei;
 - ii. Kuitaka IGUWASA kuwasilisha ratiba ya utekelezaji wa hatua zinazolenga kupunguza NRW, ikionesha idadi ya mita zitakazobadilishwa, maeneo yatakayowekewa DMAs, kilomita za mabomba zitakazokarabatiwa, gharama na muda wa utekelezaji;
 - iii. Kujiridhisha kuwa makadirio ya kiasi cha maji kinachotarajiwa kutozwa bili yanaendana na malengo halisi na yanayotekelezeka ya kupunguza NRW;
 - iv. Kufuatilia utekelezaji wa uwekezaji unaolenga kupunguza NRW sambamba na matokeo yake, ili kuhakikisha kuwa gharama zinazobebwa na watumiaji zinatafsirika katika maboresho yanayopimika ya ufanisi wa mfumo; na
 - v. Pale ambapo uwekezaji ulioruhusiwa kupitia bei umetekelezwa lakini malengo ya NRW hayajafikiwa, kuitaka IGUWASA kueleza sababu za kutofikiwa kwa malengo hayo na hatua za kurekebisha hali hiyo, na taarifa hizo zizingatiwe katika tathmini ya gharama na mapitio ya bei yanayofuata.
9. Mpango Biashara umeweka lengo la kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato kutoka asilimia 95 hadi asilimia 99 ifikapo Juni 2031, na umeainisha kuimarisha ushirikishwaji wa wateja na mfumo wa kidijitali wa utoaji bili kuwa miongoni mwa shughuli muhimu za kipindi cha miaka mitano. (Business Plan, Executive Summary, uk. ix–x).

Aidha, Ombi la Marekebisho ya Bei limeainisha ufungaji wa mita za maji za malipo kabla ya matumizi 2,500, pamoja na kuboresha ufanisi wa utoaji bili na mifumo ya ukusanyaji wa mapato kuwa miongoni mwa hatua za kuongeza mapato na ufanisi wa Mamlaka. (Ombi la Marekebisho ya Bei, Sehemu ya 2.3.3, uk. 4).

Mkataba wa Utendaji unaonesha kuwa ufanisi wa utoaji bili ulikuwa asilimia 80 mwaka 2024/25 dhidi ya kiwango linganishi cha asilimia 95, huku lengo la mwaka 2025/26 likiwa asilimia 85. Mkataba huo pia unaeleza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato kuwa uwiano wa kiasi kilichokusanywa dhidi ya kiasi kilichotozwa bili. (Performance Contract,

Appendix A, KPI 2.6, uk. 13; Maelezo ya Viashiria vya Utendaji (Performance Indicators), uk. 20).

Wadau pia walieleza changamoto katika mfumo wa malipo wa e-WATER na kuomba uboreshwe. IGUWASA ilieleza kuwa imeandaa mkakati wa kuhamia kwenye mfumo wa malipo ya moja kwa moja kupitia mfumo wa malipo kabla ya matumizi. (Muhtasari wa Kikao cha Wadau cha tarehe 26 Mei 2026, uk. 6).

Baraza linaunga mkono hatua zinazolenga kuongeza ufanisi wa utoaji bili na ukusanyaji wa mapato. Kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato kunaweza kuongeza mapato ya Mamlaka bila kutegemea ongezeko la bei pekee. Hivyo, watumiaji wanaolipa bili zao kwa wakati hawapaswi kubebeshwa kupitia bei gharama zinazoweza kupunguzwa kwa kuboresha utoaji bili, ukusanyaji wa madeni na mifumo ya malipo.

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha kuhusu kiwango sahihi cha sasa cha ufanisi wa utoaji bili na ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha viashiria hivyo vinafafanuliwa na kupimwa kwa uthabiti;
- ii. Kuitaka IGUWASA kuweka malengo ya kila mwaka ya kuongeza ufanisi wa utoaji bili na ukusanyaji wa mapato pamoja na hatua mahsusi za kuyafikia;
- iii. Kufuatilia utekelezaji wa mita za malipo kabla ya matumizi na maboresho ya mifumo ya malipo ili kubaini kama yanaongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na kupunguza madeni; na
- iv. Kuhakikisha kwamba maboresho ya ukusanyaji wa mapato yanazingatiwa katika tathmini ya mahitaji ya mapato, ili ongezeko la bei lisiwe mbadala wa kuboresha ufanisi wa ukusanyaji.

10. Mpango Biashara unaonesha kuwa pamoja na mapato ya mauzo ya maji, IGUWASA inatarajia kupata mapato kupitia huduma nyingine, zikiwemo huduma ya uondoaji wa majitaka kwa lori, ada za maunganisho mapya, ada za kuunganishiwa upya na mapato mengine yanayojumuisha faini na adhabu za kifedha. Kwa mwaka 2026/27, Mpango Biashara unakadiri mapato ya huduma ya uondoaji wa majitaka kwa lori kuwa takribani

Shilingi milioni 77.905, ada za maunganisho mapya Shilingi milioni 33.053, ada za kuunganishiwa upya Shilingi milioni 4.675 na mapato mengine takribani Shilingi milioni 55.955. (Business Plan, Jedwali Na. 17, uk. 36).

Kwa upande mwingine, Jedwali la Mahitaji ya Mapato katika Ombi la Marekebisho ya Bei linaonesha kuwa kiasi kinachopunguzwa kama Mapato Mengine (Other Income) ni takribani Shilingi milioni 42 mwaka 2026/27, kabla ya kubaini kiasi cha Shilingi bilioni 9.491 kinachopaswa kurejeshwa kupitia mauzo ya maji. (Ombi la Marekebisho ya Bei, Jedwali Na. 16, uk. 23).

Baraza linaona kuwa kuwepo kwa tofauti kati ya mapato mengine yanayoonekana katika makadirio ya utendaji wa kifedha na kiasi kinachopunguzwa kama Mapato Mengine (Other Income) katika ukokotoaji wa mahitaji ya mapato kunahitaji ufafanuzi. Si lazima mapato yote yanayoonekana kwenye taarifa ya mapato yashughulikiwe kwa namna moja katika modeli ya bei, lakini ni muhimu IGUWASA ioneshe wazi ni mapato yapi yamejumuishwa katika Mapato Mengine, yapi hayajajumuishwa, na sababu zake.

Kwa kuwa kila Shilingi ya mapato halali kutoka vyanzo vingine inaweza kupunguza kiasi kinachohitajika kurejeshwa kupitia bei ya maji, upatanisho wa taarifa hizi una umuhimu wa moja kwa moja kwa watumiaji.

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuitaka IGUWASA kuwasilisha mchanganuo wa vipengele vinavyounda Mapato Mengine (Other Income) katika Jedwali Na. 16 la Ombi la Marekebisho ya Bei;
- ii. Kulinganisha mchanganuo huo na mapato ya huduma ya uondoaji wa majitaka kwa lori, maunganisho mapya, ada za kuunganishiwa upya na mapato mengine yaliyooneshwa katika Jedwali Na. 17 la Mpango Biashara;
- iii. Kuhakikisha kuwa mapato yote yanayostahili kupunguza kiasi kinachopaswa kurejeshwa kupitia mauzo ya maji yanazingatiwa ipasavyo; na

- iv. Kuhakikisha kuwa watumiaji hawabebeshwi kupitia bei inayotozwa kwa ujazo wa maji gharama ambazo tayari zinarejeshwa kupitia ada au mapato mengine ya huduma.

11. IGUWASA ina uwezo wa kutoa huduma ya maji kwa saa 24 kwa siku, isipokuwa pale kunapotokea kukatika kwa huduma kulikopangwa au kusikopangwa. Aidha, Mkataba wa Utendaji unaweka kiwango linganishi na lengo la saa 24 za huduma kwa siku. (Business Plan, Sehemu ya 2.2.12, uk. 9; Performance Contract, Appendix A, KPI 2.5, uk. 13).

Kwa upande wa ubora wa maji, Mpango Biashara unaeleza kuwa IGUWASA haina vifaa vya kutosha vya maabara kufanya vipimo vya kibakteria na kemikali zote yenyewe, na hivyo hutumia maabara ya Singida kila robo mwaka kwa baadhi ya vipimo. Hata hivyo, Mamlaka inaeleza kuwa maji yanayotolewa kwa watumiaji yanakidhi Viwango vya Uboora wa Maji Tanzania (Tanzania Water Quality Standards) (Business Plan, Sehemu ya 2.2.12–2.2.13, uk. 10).

Aidha, Annex ya malengo ya ubora wa huduma inaonesha uzingatiaji wa viwango vya ubora wa maji ya asilimia 99.4 mwaka 2024/25, asilimia 99.7 mwaka 2025/26 na lengo la asilimia 100 kuanzia 2026/27, pamoja na malengo ya muda wa kutoa taarifa kuhusu kukatika kwa huduma, urejeshaji wa huduma baada ya kukatika kwa huduma kwa dharura na muda wa kushughulikia malalamiko. (Business Plan, Appendix B, Annex B-1, uk. 45).

Hata hivyo, wadau walibainisha changamoto halisi katika baadhi ya maeneo. Wadau walieleza kuwa maji ya Igogo yanaonekana kuwa na uchafu na harufu mbaya, na kwamba maeneo ya Mwamashimba na Jogohya yanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa maji. Pia ilielezwa kuwa taarifa za mivuho wakati mwingine hazishughulikiwi kwa wakati. IGUWASA iliahidi kuboresha chanzo cha Igogo, kuandaa ratiba ya usambazaji pale inapohitajika na kuboresha mwitikio wa mafundi. (Muhtasari wa Kikao cha Wadau cha tarehe 26 Mei 2026, uk. 5–6).

Baraza linaona kuwa ongezeko la bei linapaswa kuambatana na maboresho yanayoweza kuonekana na kupimwa katika huduma. Hivyo, mafanikio ya bei mpya hayapaswi kupimwa kwa mapato ya Mamlaka pekee, bali pia kwa ubora wa maji, saa za huduma, mwitikio kwa taarifa za uvujaji na malalamiko, pamoja na uhakika wa huduma katika maeneo yenye changamoto.

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuhakikisha kuwa utekelezaji wa bei mpya unaambatana na malengo ya kila mwaka ya ubora na uhakika wa huduma;
- ii. Kufuatilia uzingatiaji wa viwango vya ubora wa maji, hususan katika maeneo yaliyotajwa na wadau kuwa na changamoto kama Igogo;
- iii. Kufuatilia saa halisi za huduma katika maeneo mbalimbali badala ya kutegemea wastani wa mfumo mzima pekee;
- iv. Kuweka viashiria vya muda wa kushughulikia taarifa kwa taarifa za mivujo na malalamiko ya wateja na kufuatilia utekelezaji wake; na
- v. Kuhakikisha kuwa mapato ya ziada yanayotokana na bei mpya yanatafsirika katika maboresho yanayopimika kwa watumiaji.

12. IGUWASA inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na tope kinyesi katika Mji wa Igunga. Mpango Biashara unaonesha kuwa mradi huo unahusisha ujenzi wa mabwawa matano ya kutibu majitaka, eneo oevu lililojengwa kwa ajili ya matibabu, barabara ya kufikia eneo la mradi, kichomea taka, uzio na nyumba ya mlinzi pamoja na huduma ya umeme. Hadi wakati wa kuandaa Mpango Biashara, utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia asilimia 48, kwa gharama ya takribani Shilingi bilioni 1.862, huku Serikali ikiwa mfadhili. (Business Plan, Appendix B, Annex B-5, uk. 50).

Mpango Biashara pia unaonesha kuwa kiwango cha upatikanaji wa huduma za usafi wa mazingira ni asilimia 41.5 na kinatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 47.0 mwaka 2030/31. Makadirio hayo yanaonesha pia tofauti katika upatikanaji wa huduma kati ya maeneo mbalimbali; kwa mfano, eneo la Igunga linatarajiwa kufikia kiwango cha upatikanaji wa huduma ya asilimia 98.1 mwaka 2030/31, wakati baadhi ya maeneo

mengine yanaendelea kuwa na viwango vya chini vya huduma. Hivyo, pamoja na kukamilisha miundombinu iliyopangwa, kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa uwekezaji huo unatafsirika katika kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma kwa watumiaji. (Business Plan, Appendix I – Sanitation Coverage Projections, uk. 57).

Kwa upande wa ada za huduma, IGUWASA inapendekeza kuongeza ada ya lori la kuondoa majitaka na tope kinyesi ya ujazo wa mita za ujazo 10 kutoka Shilingi 158,000 hadi Shilingi 189,769.81 mwaka 2026/27, sawa na ongezeko la takribani asilimia 20.1, na kufikia Shilingi 237,280.71 mwaka 2030/31, sawa na ongezeko la jumla la takribani asilimia 50.2 ikilinganishwa na bei ya sasa. Kwa lori la mita za ujazo 5, ada inapendekezwa kuongezeka kutoka Shilingi 105,000 hadi Shilingi 166,944.46 mwaka 2026/27, sawa na ongezeko la takribani asilimia 59.0, na kufikia Shilingi 212,860.01 mwaka 2030/31, sawa na ongezeko la jumla la takribani asilimia 102.7 ikilinganishwa na bei ya sasa. Wakati huohuo, ada za utupaji wa tope kinyesi zinapendekezwa kubaki Shilingi 25,000 kwa lori la mita za ujazo 10 na Shilingi 20,000 kwa lori la mita za ujazo 5 katika kipindi chote. (Ombi la Marekebisho ya Bei, Jedwali Na. 18, uk. 26).

Baraza linatambua umuhimu wa huduma za usafi wa mazingira katika kulinda afya ya wananchi na mazingira, pamoja na umuhimu wa IGUWASA kuwa na mapato yanayotosha kugharamia uendeshaji endelevu wa huduma hizo. Hata hivyo, tofauti kubwa katika kiwango cha ongezeko linalopendekezwa kati ya lori la mita za ujazo 10 na lori la mita za ujazo 5 inahitaji maelezo ya kutosha. Wakati ada ya lori la mita za ujazo 10 inapendekezwa kuongezeka kwa asilimia 20.1 mwaka wa kwanza, ada ya lori la mita za ujazo 5 inapendekezwa kuongezeka kwa asilimia 59.0 katika mwaka huo huo. Hadi mwisho wa kipindi, ada ya lori la mita za ujazo 5 itakuwa imeongezeka kwa zaidi ya mara mbili ya bei ya sasa.

Baraza linaona kuwa tofauti hiyo haipaswi kupitishwa kwa kuzingatia makadirio ya bei pekee bila kuthibitisha gharama halisi ya kutoa kila aina ya huduma. Ni muhimu kubaini iwapo tofauti hiyo inatokana na gharama za mafuta, umbali wa safari, idadi ya safari, watumishi, matengenezo, uchakavu wa magari au sababu nyingine zinazoweza kuthibitishwa. Aidha, EWURA inapaswa kujiridhisha kuwa mfumo wa bei hauleti hali

ambayo watumiaji wanaotumia lori dogo la mita za ujazo 5 wanabeba gharama kubwa isiyolingana na gharama halisi ya huduma wanayopata.

Baraza linaona pia umuhimu wa kutenganisha gharama za ujenzi wa miundombinu na gharama za uendeshaji wa huduma. Kwa kuwa mradi wa kituo cha kutibu tope kinyesi umeainishwa kuwa unafadhiliwa kupitia ruzuku ya Serikali, gharama za mradi zilizofadhiliwa kwa ruzuku hazipaswi kurejeshwa tena kutoka kwa watumiaji kupitia ada za usafi wa mazingira au bei ya maji. Hata hivyo, gharama halali na zenye ufanisi za kuendesha, kutunza na kutoa huduma baada ya miundombinu kukamilika zinaweza kuzingatiwa katika kupanga ada, baada ya kuthibitishwa.

Aidha, ongezeko la ada linapaswa kutazamwa sambamba na lengo la kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma za usafi wa mazingira. Ada ambayo ni kubwa kuliko uwezo wa watumiaji inaweza kupunguza matumizi ya huduma rasmi ya uondoaji wa majitaka na tope kinyesi, na hivyo kudhoofisha lengo la kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma na manufaa yanayotarajiwa kutokana na uwekezaji wa Serikali. Kwa hiyo, suala la uwezo wa watumiaji kumudu gharama linapaswa kuzingatiwa pamoja na urejeshaji wa gharama wakati wa kuamua viwango vya mwisho vya ada.

Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuhakiki msingi wa ukokotoaji wa ada za huduma ya uondoaji wa majitaka kwa lori kwa kila ukubwa wa lori, kwa kuzingatia gharama halisi za mafuta, watumishi, matengenezo, uchakavu, umbali na idadi ya safari pamoja na gharama nyingine zinazohusiana moja kwa moja na utoaji wa huduma;
- ii. Kuitaka IGUWASA kueleza na kuthibitisha sababu za tofauti kubwa ya ongezeko la ada kati ya lori la mita za ujazo 5 na lori la mita za ujazo 10, hususan ongezeko la asilimia 59.0 kwa lori la 5m³ dhidi ya asilimia 20.1 kwa lori la 10m³ katika mwaka 2026/27;

- iii. Kujiridhisha kuwa viwango vitakavyoidhinishwa vinaakisi gharama halisi na zenye ufanisi za kutoa huduma na havibebeshi kundi lolote la watumiaji gharama zisizolingana na huduma inayotolewa;
- iv. Kuitaka IGUWASA kutenganisha kwa uwazi gharama za uwekezaji katika miundombinu ya usafi wa mazingira, gharama za uendeshaji wa huduma na vyanzo vya fedha vinavyogharamia kila sehemu;
- v. Kuhakikisha kuwa gharama za mradi wa kituo cha kutibu tope kinyesi zilizofadhiliwa kupitia ruzuku ya Serikali hazirejeshwi tena kutoka kwa watumiaji kupitia ada za usafi wa mazingira, bei ya maji au Rate Base/ROI;
- vi. Kuzingatia uwezo wa watumiaji kumudu ada zinazopendekezwa, hususan kwa kuangalia kama kiwango cha ongezeko kinaweza kuathiri matumizi ya huduma rasmi za uondoaji wa majitaka na hivyo kuathiri malengo ya kiwango cha upatikanaji wa huduma za usafi wa mazingira; na
- vii. Kufuatilia ukamilishaji wa mradi pamoja na ongezeko la kiwango cha upatikanaji wa huduma za usafi wa mazingira ili kuhakikisha kuwa uwekezaji na ada zitakazoidhinishwa zinatafsirika katika upatikanaji, usalama na ubora wa huduma kwa watumiaji.

13. Baada ya kupitia Ombi la Marekebisho ya Bei la IGUWASA pamoja na nyaraka zingine zilizowasilishwa kuunga mkono ombi hilo, Baraza linatambua kuwa IGUWASA ina mahitaji halisi ya kifedha na kiuwekezaji yanayohitaji kushughulikiwa ili kuhakikisha huduma ya maji na usafi wa mazingira inakuwa endelevu. Ombi la IGUWASA linaonesha kuwa marekebisho ya bei yanakusudiwa kugharamia gharama za uendeshaji na matengenezo, kukarabati na kupanua miundombinu, kupunguza NRW, kukamilisha miundombinu ya usafi wa mazingira na kuboresha mifumo ya huduma kwa wateja. (Ombi la Marekebisho ya Bei, Sehemu ya 2.0–2.6, uk. 3–5; Business Plan, Executive Summary, uk. ix–x).

Hata hivyo, Baraza linaona kuwa kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho kuhusu kiwango cha bei, ni muhimu EWURA ijiridhishe kwamba kiwango cha mapato kinachotakiwa kurejeshwa kutoka kwa watumiaji kinatokana na gharama halisi, za lazima na zenye

ufanisi, na kwamba vyanzo vingine vya fedha, hususan ruzuku na mapato mengine ya huduma, vimezingatiwa ipasavyo.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA kuzingatia mambo yafuatayo:

- i. Kujiridhisha kuhusu ukubwa wa ongezeko la bei kwa kila kundi la watumiaji na kuzingatia uwezekano wa kusawazisha au kutekeleza ongezeko kwa awamu ili kupunguza mzigo wa ghafla kwa watumiaji;
- ii. Kuhakiki gharama kubwa za uendeshaji na matengenezo, hususan ununuzi wa maji kwa jumla, kemikali, umeme, matengenezo na gharama za watumishi, ili kuhakikisha zinatokana na mahitaji halisi na zinatumika kwa ufanisi;
- iii. Kufanya uhakiki wa Rate Base, WACC na ROI na kuhakikisha kuwa kiwango cha marejesho kinachoruhusiwa kinatokana na mali zinazostahili na thamani sahihi ya msingi wa uwekezaji;
- iv. Kuhakikisha kuwa mali na miradi iliyofadhiliwa kupitia ruzuku za Serikali au michango ya wahusika wengine haitumiki kuongeza marejesho yanayotozwa kwa watumiaji kwa namna isiyostahili;
- v. Kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa masharti ya Agizo la Bei lililopita na kuhakikisha kuwa shughuli ambazo hazikukamilika zinafanyiwa upatanisho wa gharama kabla ya kuingizwa katika ombi jipya;
- vi. Kufanya tathmini ya Mpango wa Uwekezaji wa IGUWASA na kuweka kipaumbele kwenye miradi inayoboresha moja kwa moja upatikanaji, uhakika na ubora wa huduma pamoja na kupunguza NRW;

- vii. Kuhakikisha utekelezaji wa bei mpya unaambatana na malengo ya kila mwaka ya kupunguza NRW kutoka asilimia 22 hadi asilimia 17 na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato;
- viii. Kuitaka IGUWASA kuoanisha mapato mengine ya huduma na kiasi kinachopunguzwa kama Mapato Mengine (Other Income) katika ukokotoaji wa Mahitaji ya Mapato (Revenue Requirement) ili watumiaji wasibebeshwe gharama ambazo tayari zinarejeshwa kupitia vyanzo vingine;
- ix. Kuhakikisha kuwa ongezeko la bei linaambatana na maboresho yanayopimika katika ubora wa maji, saa za huduma, mwikio kwa taarifa za uvujaji na malalamiko, pamoja na upanuzi wa huduma;
- x. Kujiridhisha kuhusu msingi wa ukokotoaji wa gharama za huduma ya uondoaji wa majitaka kwa lori na kuhakikisha kuwa gharama za usafi wa mazingira zinagawanywa kwa uwazi kati ya ada za huduma, ruzuku na mapato mengine; na
- xi. Kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa masharti ya bei, miradi ya uwekezaji na viashiria vya huduma katika kipindi chote cha utekelezaji ili kuhakikisha kuwa mapato ya ziada yanayokusanywa yanatafsirika katika manufaa halisi kwa watumiaji.

14. Baraza linatambua umuhimu wa IGUWASA kuwa na rasilimali za kutosha kugharamia uzalishaji na ununuzi wa maji, matengenezo ya miundombinu, upanuzi wa mtandao, kupunguza maji yasiyoingiza mapato na kukamilisha miradi ya usafi wa mazingira. Mpango Biashara unaonesha malengo ya kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia 94.5 hadi asilimia 99, kupunguza NRW kutoka asilimia 22 hadi asilimia 17, kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato kutoka asilimia 95 hadi asilimia 99 na kufikia asilimia 100 katika ushughulikiaji wa malalamiko ifikapo Juni 2031. (Business Plan, Executive Summary, uk. ix–x).

Baraza pia linatambua kuwa baadhi ya uwekezaji unaopendekezwa, kama upanuzi wa mtandao, ubadilishaji wa mita, ukarabati wa mabomba chakavu na kukamilisha kituo cha kutibu tope kinyesi, unaweza kutoa manufaa ya moja kwa moja kwa watumiaji iwapo utatekelezwa kwa ufanisi na kwa wakati. (Business Plan, Jedwali Na. 13, uk. 29; Jedwali Na. 14, uk. 30–32).

Hata hivyo, kutokana na ukubwa wa ongezeko la bei linalopendekezwa katika mwaka wa kwanza, pamoja na maeneo yanayohitaji uhakiki zaidi katika Mahitaji ya Mapato, ROI, ruzuku, gharama za uendeshaji na utekelezaji wa shughuli za kipindi kilichopita, Baraza linaona kuwa uamuzi wa bei unapaswa kufanywa baada ya kujiridhisha kuwa watumiaji wanabebeshwa tu gharama zilizo halali, za lazima na zenye ufanisi.

Kwa msingi huo, Baraza linaona kuwa bei yoyote itakayoidhinishwa inapaswa kuweka uwiano kati ya uendelevu wa kifedha wa IGUWASA, uhalali na ufanisi wa gharama, uwezo wa watumiaji kumudu huduma na maboresho yanayopimika katika huduma wanazopokea. Utekelezaji wa bei hiyo unapaswa pia kufuatiliwa kupitia malengo ya kila mwaka ya NRW, kiwango cha upatikanaji wa huduma, ubora na uhakika wa maji, ufanisi wa ukusanyaji wa mapato, huduma za usafi wa mazingira na utekelezaji wa miradi ya uwekezaji.

Naomba kuwasilisha.